UTUME WAWANAUME KATOLIKI (T)

JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

UTUME WA WANAUME KATOLIKI (T) JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

HISTORIA YA UTUME WA WANAUME WAKATOLIK (T)

1. **KIMATAIFA:**
   Utume huu ulianzishwa mwaka 1922 huko Ulaya (Austria). Hata hivyo utume huu haukuwa na nguvu sana hadi mwaka 1947 wakati Aksio Katoliki ilipofanya Jubilee ya miaka 25 na kufanya mkutano maalum. Wajumbe walioshiriki katika mkutano huo walishauriana kuunda kamati maalum ya kuandaa katiba rasmi. Mwaka 1948, kamati hiyo ilianza kushughulikia katiba.
   Mnamo tarehe 15 hadi 17 Agosti 1950 Baraza kuu la kwanza la Kimataifa la Wanaume Katoliki (International Council of Catholic Men) lilikutana huko VATICAN. Wakati huo Baba Mtakatifu Papa Pio wa XII aliidhinisha utume huu na kuuita "UNUMONES" kama rejeo la Injili ya Yohana 17:22 ……." Ili wawe na umoja kama sisi tulivyo na umoja"Papa Pio XII aliteua utume huu uwe na Makao Makuu yake Vatican na ndiyo utume pekee wenye Makao Makuu yake VATICAN. Baadaye utume huu ulianza kuenezwa sehemu nyingi Ulimwenguni na hasa Ulaya. Hivyo ulionekana umuhimu wa kuuneza utume huu katika sehemu nyingine na Afrika ikiwa mojawapo.

2. **AFRIKA:**
   Kufuatia hoja hiyo ya kuanzisha utume huo Afrika, Viongozi wa Baraza la Kimataifa la Wanaume Katoliki (International Council of Catholic Men) I.C.C.M waliitisha kikao chao huko Nairobi tarehe 14 hadi 16 Agosti, 1983. Wakati wa mkutano huo mada nyingi zilitolewa. Maaskofu wengi kutoka Afrika kama vile Askofu Peter Dery (Jimbo la Tamare – Ghana) Askofu Silas S. Njeru (Jimbo la Meru – Kenya) Bwana Lazarius Masipeta (Kutoka Zambia) na Padri Joseph Osei (Katibu Mkuu wa Shirikisho la Mabaraza la Maaskofu wa Africa na Madagascar (SECUM). Mkutano huu ulihudhuriwa pia na Walei kutoka Tanzania, hapo ndiyo vuguvugu la kuanzisha utume lilipoingia Tanzania.

3. **TANZANIA:**
   Mwaka 1985 utume huu ulianzishwa kwa mara ya kwanza katika jimbo la Bukoba. Mwaka 1986 mwezi Septemba utume huu ulianzishwa katika jimbo kuu la Dar es Salaam. Jitihada zinaendelea kufanyika kuanzishwa matawi katika Majimbo mengine ya Tanzania. Mpaka sasa Majimbo yalioanzisha Utume huu ni Bukoba, Geita, Dar es Salaam, Mwanza, Kahama, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Morogoro, Arusha, Tanga, Songea, Lindi, Iringa, Mbeya na Kilimanjaro.

4. **UTUME WA WANAUME KATOLIKI NI NINI?**
   Utume wa Wanaume Katoliki ni utume wa UTENDAJI KATOLIKI (AKSIO KATOLIKI), kwa hiyo ni utume unaotambua kazi na shabaha za utendaji katoliki kulingana na Mtaguso Mkuu wa Vaticano II. Katika kazi zake utume wa Wanaume Katoliki hauhusiani na vyama vya siasa, wala mashirika yenye kuhusika na mahitaji/misaada. Ni utume wenye lengo kuu la mashirika yenye kuhusika na mahitaji/misaada. Ni utume wenye lengo kuu la kutangaza Neno la Mungu kwa

mataifa yote, kwa mfano mwema wa familia, Jumuiya na kumtumikia Mungu na katika jumuiya ambamo Mwanautume anaishi. Wanaume Katoliki ni chachu duniani. Utume wa Wanaume Katoliki ni muungano wa wanaumwe wa Mataifa katika muundo ambao husaidia na kushiriki katika kufahamu umoja wa ulimwengu, ujenzi wa dunia ya haki, kustawisha na kutoa misaada ya kimisionari katika hali inayoelekeza kukuza hali ya "ndugu mhitaji" brother in need.

5. NANI AENDESHE UTUME WA WANAUME KATOLIKI?

Utume wa Wanaume Katoliki huendeshwa na wanaume

- Ambao huishi kulingana na imani yao.
- Walio na msimamo imara kwa Kanisa Katoliki.
- Ambao wanahamu ya kuishi maisha ya kikristu katika ndoa, Jumuiya, Jamii, Kazini na kutenda vitendo vya kitume wakizingatia kusali kwa kujitoa muhanga (pray with devotion).
- Ambao wana hamu ya kufanya upya imani yao na wanaojaribu kutafuta njia ya kuamsha nia hiyo.
- Ambao hushughulikia binadamu hasa nyakati za shida.
- Ambao huelewa kwamba usawa na binadamu na haki ni tatizo kubwa ulimwenguni, kwa hiyo wanaona haja ya kupendana, kupatana na kusaidiana katika mataifa.
- Ambao wanajitolea kuleta mawazo mema mahali popote wanapohitajika katika imani ya ukristu.

6. UTUME WA WANAUME KATOLIKI UNAHITAJI NINI?

(i) Kutubu na kujitolea kwa mtu binafsi.

- Kazi ambayo Utume wa Wanaume Katoliki hujitoea kuihubiri injili, Kushiriki wadhifa wa Kikuhani, Kinabii, katika Ufalme wa Kristu katika taiza zima la Wakristu na Ulimwengu. (Lumen Centium Na. 3) Kila Mwanaume ashughulike na
- Huduma za kanisa ambako jamii ya Kikristu huundwa kwanza (Jumuiya Ndogondogo za Kikristu).
- Katika sehemu za Parokia ambako jamii huishi.
- Katika Mashule na sehemu nyingi za elimu ambako watu hurekebishwa tabia.
- Sehemu za Kazini na Biashara
- Katika Siasa.
- Katika utamaduni na nyakati za mapumziko baada ya kazi.

(ii) Kutegemeza Kanisa

Kikundi kama msingi wa jamii katika Utume wa Wanaume Katoliki hulenga kuamsha bidii, kukusanya na kuweka nguvu na kufanya kazi pamoja kwa nia ya kuleta maendeleo ya jumuiya wanamoishi kwa lengo la kutegemeza kanisa na Wanautume wake.

- Kwa kuvuta wanaume kufanya kazi za maendeleo kama miradi.
- Kuendesha mafundisho ya dini kwa wale wanaohitaji.
- Kwa kusaidia jamii wanamoishi.

(iii) Ushirikiano

Roho Mtakatifu anatufanya sisi tuzingatie wajibu wetu zaidi kama wanaume na kutuhimiza kumtumikia Kristu kwa ushirikiano. Wito wa pekee kwetu sisi sote ni kuutafufa Ufalme wa Mbingu kwa njia ya kushughulikia malimwengu na kuyaongoza kwa ushirikiano kadri ya mapenzi ya Mungu.

Kwa hiyo, Utume wa Wanaume Wakatoliki unashirikiana na Parokia Kamati tendaji na Vyama vingine vya Kitume, wakisaidiana kuchukua, kutoa mawaidha na kuendeleza kauli za viongozi wa hiarakia.

(iv) Kumuelekea Kristu katika hali ya maisha

- Kwa kuchunguza hali ya maendeleo ya kijamii, hasa wakati huu wa Sayansi na Tekinolojia ambapo kuna ukiukwaji wa maadili kwa kutumia vibaya vifaa vya mawasiliano na kupashana habari.
- Kwa kushauri mambo yanayohusu nchi, siasa, utamaduni na elimu kulingana na matakwa ya kanisa.
- Kuwapa moyo wa kushiriki katika maendeleo ya Taifa wakizingatia wajibu wao kama Wakatoliki kwamba wameitwa na Mungu kuwa chachu ulimwenguni kwa njia ya kazi zao za kiume wakijibidisha kwa Roho ya Kikristu.

7. UTUME WA WANAUME WAKATOLIKI HUFANYA KAZI NAMNA GANI

Mtu binafsi anaweza kufanya mengi, lakini anaweza kufanya mengi zaidi katika jamii. Kwa hiyo, Utume wa Wanaume Katoliki unahimiza ushirikiano uwe ni lazima katika vikundi vilivyomo. Ni muhimu sana kuwe na Utume wa Wanaume Katoliki katika Jumuiya Ndogondogo za Kikristu, Kigango/Kanda, Dinari, Jimbo na Kitaifa. Hivyo Utume hauwezi kufanya kazi zake katika ngazi ya Parokia peke yake tu. Kwa hiyo Utume hutumia njia, mipango (Kimataifa) ya kutafuta mambo yanaoweza kufanyika katika Parokia, Dinari Jimbo na Taifa.

Ni kazi ya Utume wa Wanaume Katoliki kuimarisha shabaha ya kazi kwa viwango tofauti. Mtaguso Mkuu wa Vaticano II, unatoa amri kwa Mitume sehemu ya IV sura ya 20 inaseme hivi.-

Mipango hii ya kitume kama inaitwa ya Utendaji Katoliki (Aksio Katoliki) ama kitu kingine ambacho katika nyakati zetu kinaonyesha kazi za kitume za hali ya juu, hutambuliwa kwa mambo yafuatayo-:

(a) Shabaha ya kwanza ya Utume huu ni ile ya kitume kwa kanisa na hivyo kujielekeza kwa Mungu na kuwasaidia watu wajifahamu katika ukristu ambao unawasaidia, waingize Neno la Mungu kwa jamii nyingi na mazingira tofauti wakiwa na Roho ya Mungu.

(b) Washiriki (waamini) hushirikiana kwa njia zo dhahiri na utawala wa kanisa, hufanya kazi kutokana na uwezo wao na kuchukua majukumu katika uongozi huu wa kitume hali hii hufafanua zile kazi za kichungaji wa kanisa ambazo ni lazima ziendeshwe pia katika kupanga na kufahamu orodha ya vitendo.

(c) Kazi za watu huendeshwa na nguvu zilizounganishwa pamoja kama viungo vya mwili ili ieleze wazi jamii ya kanisa na hivyo ifanye utume uenee imara.
(d) Watu wanaojitolea kwa hiari yao ama wanaoalikwa kushirikiana na kufanya kazi pamoja na utawala wa kitume, wanafanya hivyo chini ya uongozi bora na utawala wenyewe. Utawala wa Askofu unaweza kuthibitisha ushirikiano na agizo wazi.
(e) Vyama ambavyo tabia hizi zinaweza kupatikana pamoja kulingana na uamuzi wa utawala wa Askofu, vinachukuliwa kama kikundi cha Utendaji Katoliki hata vikiwa na majina na miundo tofauti kwa sababu ya mahitaji, mazingira na nchi kwa ujumla.

8. SERA YA MAENDELEO YA UTUME WA WANAUME WAKATOLIKI

MSINGI WA SERA

Kuwaendeleza wanaume KIROHO na KIMWILI

Sera itasisitiza kuwashirikisha wanaume katika maendeleo yao. Utume wa Wanaume Katoliki (UNUM-OMNES) hautalenga kuwaendeleza wanaume bali kuwasadia wajiendeleze ili wategemee Utume na Kanisa lao kwa kutoa michango yao ya hali na mali.

Kwa hiyo mipango ya maendeleo itapangwa kuanzia Parokiani hadi Jimboni wakisaidiwa na uongozi wa Taifa.

Katika kufanikisha hayo bodi zifuatazo zitasimamia:

(a) Kamati ya Maendeleo ya Parokia
(b) Bodi ya Maendeleo ya Dinari
(c) Bodi ya Maendeleo ya Jimbo
(d) Bodi ya Usimamizi (Supervisory board) ya Taifa na Halmashauri ya utekelezaji ya Taifa.

(a) Kamati ya Maendeleo ya Parokia

- **Uongozi:**
  - (i) Itaongozwa na Kamati ya Utendaji ya Parokia
  - (ii) Itasimamiwa na Mwenyekiti wa miradi akisaidiwa na Katibu

- **Kazi zake:**
  - (i) Itaanzisha miradi midogo midogo ya kutegemeza Tawi na Parokia
  - (ii) Itafanya shughuli zake kadri itakavyoelekezwa na kamati tendaji na Wanaume au Wadau wa Hisa.
  - (iii) Mradi unaweza kuanzishwa kitawi au na Wanaume wachache waliochanga kuanzisha mradi. Hata hivyo Wanaume wengine wanaweza kujiunga kufuatana na utaratibu utakaowekwa na Bodi ya Maendeleo ya Jimbo hilo.

(b) Bodi ya Maendelo ya Dinari

- **Uongozi:**

  (i) Itaongozwa na Bodi ya Maendelo ya Dinari chini ya "Coordinator" wa Dinari.

  (ii) Itasimamiwa na "Coordinator" wa Dinari na Msaidizi wake.

  Watakaokuwemo kwenye Bodi hii ni.

  - ✓ Wenyeviti wa kamati za Maendeleo za Parokia
  - ✓ Wenyeviti wa kamati za Utendaji za Parokia
  - ✓ Makatibu wa kamati za Utendaji za Parokia

- **Kazi zake (Deanerian Coordinator)**

  (i) Kubuni miradi ya Dinari wakishiriana na Parokia

  (ii) Kusimamia miradi wakishirikian na Parokia

  (iii) Kutathmini miradi

  (iv) Kufungua Matawi na kufuatilia ustawi wake

(c) Bodi ya Maendeleo ya Jimbo/Jimbo kuu:

- **Uongozi:**

  (i) Itaongozwa na kamati ya utendaji ya jimbo ikisaidiana na Askofu au Mwakilishi wake.

  (ii) Itasimamiwa na Diocesan/Archiocesan Planning and Development Coordinator

  (iii) Itawajibika kwa kamati tendaji ya Jimbo

- **Kazi zake:**

  (i) Kubuni miradi na kuandaa "project write up"

  (ii) Kutafuta Wafadhili ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na viongozi wa Jimbo na Taifa kwa ushirikiano na Askofu wa Jimbo hilo.

  (iii) Kusimamia utekelezaji wa miradi na maendeleo ya idara.

  (iv) Kutathmini maendeleo ya (iii)

  (v) Kufuatilia maendeleo ya miradi ya Parokia na Dinari

MUUNDO WA BODI YA JIMBO

(i) Archdiocesan / Diocesan Planning and Development Coordinator (Chair)
(ii) Asistant APDC
(iii) Deanerian Development Coordinator
(iv) Idara ya Afya
(v) Idara ya Ustawi wa Jamii
(vi) Idara ya Elimu na Mafundisho ya Dini
(vii) Idara ya Wasiojiweza
(viii) Idara ya Vijana
(ix) Idara ya Duka na miradi
(x) Idara ya Semina, Warsha na Magazeti
(xi) Wawakilishi wa Parokia (Kila Parokia mtu mmoja)
(xii) Katibu wa Bodi anayeteuliwa na kamati tendaji ya Jimbo

N.B:

(a) Kila jimbo lizingatie kwamba lazima kupata Mtaalam wa kutembelea sehemu mbalimbali za jimbo ili kujua matatizo ya jimbo kabla ya kazi kuanza. (Economist Planner)

(b) Inapendekezwa kwamba miradi ya kuuza vitabu, daftari, rozari n.k ianzishwe na kila Parokia mara moja kabla ya miradi mingine kuanzishwa kufuatana na utaratibu ulioelezwa awali.

(c)Kila idara itakuwa na Mkuu atakayeteuliwa na Mwenyekiti au Coordinator wa Jimbo kufuatana na Utaalam wake si kwa njia nyingine nje ya hiyo.

MSIMAMO: (MOTTO WA WANAUME KATOLIKI)

KUMTUMIKIA MUNGU, KANISA, FAMILIA NA JUMUIYA ZETU

KAZI ZA VIONGOZI KATIKA UTUME WA WANAUME KATOLIKI (T)

1. MWENYEKITI

Huyu hushika uongozi wa tawi la Sub Parish, Parokia, Jimbo au Taifa. Kwa hiyo awe mtu mwenye uwezo wa kuwamudu watu. Kazi zake ni:

(a) Kuongoza mijadala katika mikutano akizingatia mambo yafuatayo:
  (i) Kuwahi kwenye vikao vya mikutano.
  (ii) Kuzingatia muda uliopangwa katika ratiba
  (iii) Kutoa nafasi sawa ya kuzungumza kwa kila msemaji au mtoa hoja bila upendeleo wa pekee. (Kufuata dondoo zilizoandaliwa)
  (iv) Kuheshimu na kupokea maoni ya wengi (Demokrasia)
  (v) Kutumia lugha safi, maelezo sahihi na mifano inayofaa.

(b) Kutayarisha dondoo kwa kushirikiana na viongozi wa kamati tendaji na hasa Katibu.

(c) Kutoa neno au uamuzi wa mwisho katika masula fulani kadri ya busara yake.

(d) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yakiwemo yatokanayo.

(e) Kupokea maelezo (miongozo ya viongozi wa kanisa (Papa, Maaskofu na Mapadre)

(f) Kutoa taarifa ya Utume wa Wanaume Katoliki katika vipindi mbalimbali (Periodical)

(g) Kuwakilisha Utume katika mialiko mbalimbali hasa ya kilei.

2. MAKAMU MWENYEKITI:

(a) Kwa ushirikiano na Katibu, kumsaidia Mwenyekiti katika shughuli zote za uongozi. (Huyu ni msaidizi mkuu wa Mwenyekiti)

(b) Kuchukua nafasi ya uongozi wa Uenyekiti kwa kuzifanya shughuli zote za uongozi wa Mwenyekiti wakati hayupo, isipokuwa zile ambazo kanuni haziruhusu kwa kutumia busara yake.

(c) Kupokea na kutekeleza maelekezo ya Mwenyekiti.

3. KATIBU:

Huyu ni mtendaji mkuu ngazi yoyote ya Utume wa Wanaume Katoliki. Kwa hiyo kwanza awe na sifa ya ujuzi wa kanuni, historia ya Utume. Awe na uwezo wa kusoma na kuandika. Awafahamu wanaumoja wote na ikiwa ni pamoja na tabia zao pale inapobidi.

Majukumu yake ni:

(a) Kuijua, kuieleza kwa ufasaha na kutumia kanuni kwa busara bila kupoteza lengo.

(b) Kushauriana na Mwenyekiti ili mawazo yao yalingane.

(c) Kuwaheshimu Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Msaidizi, Mweka hazina na wanakamati ili kuwe na uelewano kati yao.

(d) Kutunza SIRI za viongozi wa kamati tendaji na viongozi wa kanisa (Maaskofu na Mapadre).

(e) Kutayarisha dondoo za mikutano akishirikiana na viongozi wengine hasa Mwenyekiti.

(f) Kuitisha vikao kwa kutoa taarifa siku kadhaa kwa mujibu wa kanuni na kuwaarifu viongozi wanaohusika.
(g) Iwapo kuna semina, kuwaandaa wakufunzi na wageni rasmi wa kufungua na kufunga kwa kushirikiana na viongozi wenzake.
(h) Kuwakaribisha wageni.
(i) Kuandika muhtasari wa vikao na kuwasomea wajube kwenye vikao
(j) Kushughulikia barua za kiofisi
(k) Kuhifadhi na kutunza kumbukumbu zote.

4. KATIBU MSAIDIZI:

(a) Kumsaidia Katibu bega kwa bega katika kazi zote za ukatibu
(b) Kuchukua nafasi ya utendaji wote wakati katibu hayupo kwa kutumia busara yake.

5. MTUNZA HAZINA:

Sifa kubwa ya Mtunza Hazina ni kuwa MWAMINIFU, pili ajue kusoma, kuandika na uwezo wa mahesabu.

Wajibu wake ni:

(a) Kutunza mali za utume
(b) Kubuni mbinu na mipango ya kuzalisha mali kwa kushirikiano na viongozi wenzake.
(c) Kuweka hesabu vizuri na mapato na matumizi,
(d) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio yahusuyo fedha, miradi n.k
(e) Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya vitu katika vikao vinavyohusika.

6. MJUMBE/MWANAKAMATI:

Kila mmoja wa hao watatu, nafasi yake ni kuwa kiungo (mediator) kati ya uongozi na utume. Basi, wanawajibika kama ifuatavyo:

(a) Kuwakilisha mawazo ya Wanaume mkutanoni na kuwapelekea taarifa sahihi toka mkutanoni ili wajiandae kwa kikao kijacho.
(b) Kushiriki kikamilifu mijadala yote bila kukosekana na kutoa taarifa iwapo italazimu kutokuwepo mkutanoni.
(c) Kuwajibika katika majukumu ya pekee anayoteuliwa kuyafanya kama kazi za kamati au utafiti n.k.

N.B:

Wakati wa mikutano, Kamati tendaji kamwe isimiliki na kutawala mijadala bali wawe wa mwisho na Mwenyekiti atoe kauli ya mwisho.

Kama Utume mwingine na Kitume Utume wa Wanaume Wakatoliki (T) lengo lake kuu ni UMOJA KATIKA KUTAKATIFUZA MALIMWENGU KWA AJILI YA WOKOVU WA WATU.

Kila mwanaume anawajibika kueneza Utume wake kwa sala na sadaka, juhudi na maarifa

UTUME WA WANAUME KATOLIKI
UNUM OMNES

1. **UTANGULIZI:**
   Kwa sifa kama Mkristu, Mkatoliki anayo tayari madhumuni na majukumu kutokana na amri za Mungu na za Kanisa. Hii ni pamoja na kujishughulisha na utumishi wa Kanisa, kutekeleza wajibu katika familia na jumuiya anamoishi. Kushirikiana na vyama vingine vya kitume ambavyo vimeundea ili kusaidiana kuhimiza utekelezaji wa majukumu hayo.

2. **JINA:**
   Jina la Utume huu litakuwa UMOJA WA WANAUME KATOLIKI (UNUM OMNES) "UWAKA"

3. **ANUANI:**
   Ofisi ya Utume wa Walei
   S. L. P. 137,
   DAR ES SALAAM.

4. **MADHUMUNI:**
   1. Kuwaunganisha wanaume Katoliki wote ambao wana nia, moyo na ari ya kulitumikia Kanisa ili waweze kufanya kazi katika shughuli mbalimbali za utume wa Kanisa ambazo zinahitaji nguvu, maarifa, ujuzi na juhudi za pekee za kiume.
   2. Kuhifadhi, kuimarisha na kulinda imani ya Kikatoliki na pia kuendeleza elimu na mafunzo ya dini kwa watoto wakatoliki na wale wanaohitaji.
   3. Kuonyesha na kudhihirisha utii na uaminifu wao kwa Baba Mkatifu, Maaskofu na Mapadre.
   4. Kutegemeza Parokia zao kwa hali na mali katika shughuli zake za kiroho na kimwili.
   5. Kushirikiana na vyama vingine vya kitume na mashirika mengine ya kikatoliki yaliyo ndani na nje ya Tanzania.
   6. Kujishughulisha na maendeleo ya kiroho na kimwili ya wanachama wake na pia kutoa msaada kwa wale wanaohitaji na wanaostahili kwa mfano wasiojiweza, yatima na wajane.
   7. Kuhimiza kushauri na kutoa mafundisho ya uongozi pale panapowezekana na kwa wale wanofaa ili nao waweze kuingia na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya taifa.
   8. Kuhimiza kushauri na kutoa mafundisho ya uongozi pale panapowezekana na kwa wale wanaofaa ili nao waweze kuingia na kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya taifa.

5. KAMATI NDOGONDOGO

Kutakuwa na kamati ndogondogo zitakazosaidia kukamilisha madhumuni yaliyotajwa hapo juu kama ifuatavyo:

(i) Kamati ya elimu na mafundisho ya dini
(ii) Kamati ya mahusiano na usalama wa kanisa
(iii) Kamati ya uchumi na fedha
(iv) Kamati ya afya

6. KUJIUNGA KATIKA UTUME:

Sifa zinazotakiwa ili kujiunga na utume huu ni kwa mwanaume yeyote Mkatoliki mwenye umri kuanzia miaka kumi na nane (18)

7. KUONDOKA KATIKA UTUME:

Kurudi kutakuwa kwa hiari hasa mhusika atakapoacha kushirikiana na wenzake kwenye vikao na shughuli mbalimbali za utume.

8. KURUDI KATIKA UTUME:

Mhusika ataonekana karudia utume wake mara atakapoanza kushirikiana na wenzake katika vikao na shughuli mbalimbali za utume.

9. UONGOZI:

Umoja utaongozwa na Kamati Tendaji kwa ngazi zote kuanzia Jumuia Ndogondogo, Parokia hadi Jimbo. Kamati hizo zitaundwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Mweka hazina. Aidha kutakuwa na Mlezi wa Utume katika ngazi zote.

10. MIKUTANO:

Utume huu utakuwa na vikao katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:

A. Jumuiya ya Parokiani:

(i) Kutakuwepo na mkutano wa Wanachama wote kila baada ya miezi mitatu
(ii) Kutakuwepo mkutano wa Kamati Tendaji kila mwezi mara moja.
(iii) Kutakuwepo mkutano Mkuu mara moja kwa mwaka.
(iv) Kutakuwepo mkutano Mkuu wa Uchaguzi mara moja kwa miaka mitatu.
(v) Taarifa ya mkutano itakuwa ni ya wiki mbili

B. Jimboni:

(i) Kutakuwepo Mkutano wa Halmashauri ya Utekelezaji mara moja baada ya miezi mitatu.
(ii) Kutakuwepo Mkutano Mkuu wa Halmashauri ya Utekelezaji mara moja kwa mwaka
(iii) Kutakuwepo na Mkutano Mkuu wa Uchaguzi mara baada ya miaka mitatu

(iv) Kutakuwepo Mkutano wa Kamati Tendaji mara moja kwa miezi mitatu.

(v) Mkutano Mkuu wa JIMBO utahudhuriwa na wafuatao:

- Wajume wote Kamati Tendaji ya Jimbo
- Kamati Tendaji zote za Parokia yaani viongozi watano
- Mshauri / Mkurugenzi wa Jimbo (Utume wa Walei)

Muda wa kuitisha vikao ni siku ishirini na moja (21)

11. KAZI ZA VIKAO

1. Jumuiya / Parokia:

1.1 Kupokea na kujadili taarifa za kamati na vikundi vilivyopewa kazi maalum

1.2 Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji shughuli mbalimbali za utume.

1.3 Kutathmini maendeleo ya ngazi husika

2. Jimboni:

2.1 Kupokea na kujadili taarifa za kutoka Parokiani

2.2 Kujadili maendeleo ya utume JIMBONI

2.3 Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji shughuli mbalimbali za Utume.

12. KAZI ZA MIKUTANO MIKUU:

1. Jumuiya / Parokia:

1.1 Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za muhutasari wa mkutano uliopita

1.2 Kupokea taarifa za vikundi na Utume ngazi husika

1.3 Kupokea na kupanga mapato na matumizi ya Utume kwa kipindi kijacho

1.4 Kupanga malengo ya ngazi husika kadiri ya maelekezo kutoka juu

2. Jimbo:

2.1 Kusoma na kuthibitisha ukamilifu na usahihi wa mkutano mkuu uliopita

2.2 Kupokea taarifa ya utendaji ngazi zote husika.

2.3 Kupanga malengo ya Utume kwa kipindi kijacho

13. WAJIBU WA KAMATI TENDAJI.

1. Kwenye ngazi za Jumuiya, Mitaa na Parokia wajibu wa Kamati Tendaji utakuwa:
2. Kusoma na kuthibitisha kumbukumbu za kikao kilichopita.
3. Kufuatilia utekelezaji wa maamuzi na kutathmini malengo ya Utume
4. Kuhakikisha kwamba Kanuni za Utume zinafuatwa na kila mmoja.

14. MAPATO:

(a) Mapato ya Utume yanatokana na:

(i) Michango

(ii) Misaada kutoka kwa wafadhili

(iii) Shughuli mbalimbali kama zitakavyoamuliwa mara kwa mara

(b) Utunzaji Wa Fedha:

1. Fedha zote zitapokelewa na Mweka Hazina kwa kutolewa stakabadhi. Msaada wa Katibu utatumika endapo Mweka Hazina hatakuwepo.
2. Fedha itawekwa na Paroko, Parokiani au Mhasibu wa Jimbo kwa ngazi ya Jimbo.
3. Mdhamini wa fedha na mali za Utume atakuwa Paroko (Parokiani) au Mkurugenzi wa Jimbo/Mlezi ngazi ya Jimbo
4. Malipo yote yatalipwa kwa idhini ya Halmashauri

15. UCHAGUZI WA VIONGOZI

Kanuni na taratibu zote za uchaguzi zinazotumiwa na Halmashauri Walei Jimbo Kuu la Dar es Salaa zitafuatwa.

16. MAREKEBISHO YA KANUNI:

Marekebisho ya Kanuni hizi yataweza kufanyika kwa mujibu wa matakwa ya wanachama/wanaume kwa kadiri itakavyohitajika.